

Minnesota Yazindua Kampeni ya Upimaji kwa Vijana kwa Mwaka wa Shule: Nakala

[muziki unao changamsha]

[ujumbe kwenye skrini] Kile wanafunzi wanasema kuhusu upimaji wa mara kwa mara wa COVID-19.

[mwanafunzi wa 1 wa kike] Kwangu mimi kupimwa ili niwe na sherehe ya kuhitimu msimu huu wa machipuko ni muhimu sana kwangu.

[mwanafunzi wa 2 wa kike] Kwa ajili ya spoti yangu, ili niweze kushiriki na kushindana.

[mwanafunzi wa 1 wa kiume] Ninataka kuwa kwenye jukwaa la muziki wangu wa mwaka mwandamizi na tamasha la densi iitwayo 'prom' na kuhitimu.

[ujumbe kwenye skrini] Idara ya Afya ya Minnesota inapendekeza kwamba watoto na familia zao wapimwe kila baada ya wiki mbili. Watoto wanaoshiriki katika shughuli zozote za ziada au spoti, wanapaswa kupimwa kila wiki.

[Msimamizi wa Anoka, David Law] Mpango huu wa kufanya upimaji kwa wanafunzi wasipo onyesha dalili huongeza uwezekano wa kuwa tunapata asilimia ndogo sana ya wanafunzi ambao wanapatikana kuwa na virusi, na kuondoa usumbufu mkubwa kwa shughuli hiyo ya nje ya darasa au siku hiyo ya shule.

[ujumbe kwenye skrini] Upimaji sio gharama kwako, na unaweza kupanga miadi kwa familia nzima kwa wakati mmoja.

[mwanafunzi wa 1 wa kike] Sitaki kuwa msambazaji wa virusi katika jamii kwa hivyo kuja Amory, kupimwa bila malipo imekuwa rahisi. Na inahakikisha kuwa niko salama na vilevile ninaweka marafiki wangu salama.

[mwanafunzi wa 2 wa kiume] Tunataka kurudia masomo ya ana kwa ana, na tunahitaji kufanya kazi pamoja ili kufikia hatua hiyo.

[ujumbe kwenye skrini] Kuchukua tahadhari kama kuvaa barakoa na kupimwa husaidia kuzuia kuenea kwa COVID-19. Tembelea mn.gov/covid19 leo upate maelezo zaidi na upange upimaji wa familia yako.

[muziki unao changamcha]

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

3/17/21 (Swahili)

Ili kupata maelezo haya kwa muundo tofauti, piga simu kwa: 651-201-4989